Kujaribiwa Kwa Yesu

(The Temptation Of Jesus)

Na

Ellis P. Forsman

Kujaribiwa Kwa Yesu
(The Temptation Of Jesus)

Na

Ellis P. Forsman

Oktoba 15, 2011

Kujaribiwa Kwa Yesu

Mat. 4:1-11

Moja ya Baraka ya kuwa na Yesu kama Mwokozi wetu ni uwezo wake wa kutufariji na kuwasaidia wale wanaojaribiwa.

Hii ni kwa sababu naye alijaribiwa.

Heb. 2:18, "*Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa.*"

Anahuruma, na aweza kutoa msaadaa wakati wa hitaji.

Heb. 4:14-16, "*Basi iwapo tunaye kuhani mkuu aliyeingia katika mbingu, Yesu Mwana wa Mungu, na tuyashike sana maungamo yetu. Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote, bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri ili tupewe rehema, na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.*"

Moja ya wakati wake mkuu aliojaribiwa ulikuwa ni mwanzo wa huduma yake ya hadharani.

Ghafla ikafuatia ubatizo wake na Yohana.

Mat. 3:13-17, "*Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana ili abatizwe. Lakini Yohana alitaka kumzuia akisema, mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua akija juu yake; na tazama sauti kutoka mbinguni ikisema, huyu ni Mwanangu mpendwa wangu ninayependezwa naye.*"

Kabla ya kuanza huduma yake ya kuhubiri.

Mat. 4:12-17, "*Basi Yesu aliposikia ya kwamba Yohana amefungwa alikwenda zake mpaka Galilaya; akatoka Nazareti, akaja akakaa Kapernaumu, mji ulioko pwani, mipakani mwa zabuloni na Naftali; ili litimie neno lililonenwa na nabii Isaya akisema, nchi ya Zabuloni na nchi ya Naftali, njia ya bahari ng'ambo ya Yordani, Galilaya ya mataifa, watu wale waliokaa katika giza wameona mwanga Mkuu, nao waliokaa katika nchi na uvuli wa mauti mwanga umewazukia.tokea wakati huo Yesu*

alianza kuhubiri akisemaa, tubuni; kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia."

Kujifunza "Kujaribiwa Kwa Yesu" inaweza kuwa na matunda kwa sababu kadhaa...

- Inatukumbusha kwamba Yesu anaelewa majaribu yetu wenyewe.
- Inatufunualia jinsi tunavyoweza kufanikiwa katika kuyashinda majaribu.

Tukiwa na hilo katika akili zetu na kutumia Mat. 4:1-11 kama kifungu chetu kikuu, ebu tuanze na...

Kujaribiwa kwa Yesu kunaangaliwa

Mpangilio wa kujaribiwa...

Yesu aliongozwa na Roho hadi katika nyika.

Mat. 4:1, "*Kisha Yesu alipopandishwa na Roho nyikani ili ajaribiwe na Ibilisi."*

Ilikuwa ikionekana kama nyika ya Yudea, sehemu ya jangwa kuweza kujaribiwa na Ibilisi.

Ambapo Yesu alifunga na akajaribiwa kwa siku arobaini.

Mat. 4:2, "*Akafunga siku arobaini mchana na usiku, mwisho akaona njaa."*

Kufunga kwake ni kama ile ya Musa na Eliya.

- Kut. 34:28, "*Naye alikuwa huko pamoja na BWANA siku arobaini na masiku yake; hakula chakula, wala hakunywa maji. Naye akaandika katika hizo mbao, hayo maneno ya maagano, hizo amri kumi."*
- 1 Fal. 19:8, "*Akainuka, akala, akanywa, akaenda katika nguvu za chakula hicho siku arobaaini mchana na usiku, hata akafika Horebu mlima wa Mungu."*

Luka anafunua kwamba majaribu yalitokea kwa muda wa siku arobaini.

Luka 4:2, "*Akajaribiwa na Ibilisi. Na siku hizo alikuwa hali kitu hata zilipotimia, aliona njaa."*

Marko anaongelea mnyama wa porini.

Marko 1:13, "*Akawako huko jangwani siku arobaini, hali akijaribiwa na shetani; naye alikuwa pamoja na wanyama wa mwitu, na malaika walikuwa wakimhudumia."*

Ili kuwa hivyo baada ya siku arobaini ya kujaribiwa ambapo tunakuta Shetani anamwendea Yesu kwa "upeo" unaohusisha sehemu tatu za kujaribiwa.

Upeo wa kujaribiwa...

Jaribio la kwanza.

Mat. 4:3-4, "*Mjaribu akamjia akamwambia, ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu, amuru kwamba mawe haya yawe mkate. Naye akajibu akasema imeandikwa, mtu hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu.*"

Shetani anajiingiza katika tama ya mwili.

Akiwa amefunga kwa siku arobaini, kwa uasilia Yesu alikuwa na njaa.

Akiipa changamoto utambulisho wa Yesu, Shetani anajiingiza katika njaa yake ya kimwili: "*Amuru kwamba mawe haya yawe mkate.*"

Yesu anajibu kwa andiko.

Akinukuu Kum. 8:3, "*Akakutweza, akakuacha uone njaa, akakulisha kwa mana, usiyoijua wewe wala baba zako hawakuijua; apate kukujulisha ya kuwa mwanadamu haishi kwa mkate tu, bali huishi kwa kila litokalo katika kinywa cha BWANA.*"

Kuna zaidi katika maisha kuliko kutimiza tama ya kimwili; mwanadamu anategemea Neno la Mungu ili kwamba aweze kuishi!

Kujaribiwa kwa mara ya pili.

Mat. 4:5-7, "*Kisha ibilisi akamchukua mpaka mji mtakatifu, akamweka juu ya kinara cha hekalu, akamwambia, Ukiwa ndiwe Mwana wa Mungu jitupe chini; kwa maana imeandikwa, atakuagizia malaika zake; na mikononi mwao watakuchukua; usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.*"

Shetani anajiingiza katika kiburi cha uzima.

Tena akiipa changamoto utambulisho wa Yesu, Shetani anamweka Yesu juu ya hekalu, akimwambia "jirushe mwenyewe chini".

Akinukuu maandiko mwenyewe, anatumia:

Zab. 91:11-12, "*Kwa kuwa atakuagizia malaika zake wakulinde katika njia zake zote. Mikononi mwao watakuchukua, usije ukajikwaa mguu wako katika jiwe.*"

Yesu anajibu kwa andiko.

Kumb. 6:16, "*Usimjaribu BWANA Mungu wako, ...*"

Wakati kifungu alichokinukuu Shetani ni sahihi, ingeweza kuwa dhihaka kukitumia kumjaribu Mungu.

Jaribio la tatu.

Mat. 4:8-10, "*Kisha Ibilisi akamchukua mpaka mlima mrefu mno, akamwonyesha milki zote za ulimwengu, na fahari yake, akamwambia haya yote nitakupa, ukianguka kunisujudia. Ndipo Yesu alipomwambia nenda zako shetani; kwa maana imeandikwa msujudie Bwana Mungu wako, umwabudu yeye peke yake.*"

Shetani anajiingiza katika tamaa ya macho.

Akimpeleka Yesu katika kilima mlima mrefu na anamwonyesha falme za dunia.

Akimwahidi kumpa Yesu falme zote kama atamsujudia Shetani.

Yesu anajibu kwa andiko

Kum. 6:13, "*Mche BWANA Mungu wako; ndiye utakayemtumikia, na kuapa kwa jina lake.*"

Haka kama alipewa njia ya mkato kupokea uwezo juu ya mataifa, Yesu hachukui njia rahisi.

- Ufu. 2:26-27, "*Na yeye ashindaye, na kuayatunza matendo yangu hata mwisho, nitampa maamlaka juu ya mataifa, naye atawachunga kwa fimbo ya chuma, kama vyombo vya mfinyanzi vipondwavyo, kama mimi nami nilivyopokea kwa Baba yangu.*"
- Ufu. 3:21, "*Yeye ashindaye nitampa kuketi pamoja nami katika kiti change cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi.*"

Wakati wa mwisho wa kujaribiwa...

Malaika walikuja na kuhudumia Yesu.

Mat. 4:11, "*Kisha Ibilisi akamwacha, na tazama wakaja malaika wakamtumikia.*"

Walichokifanya hakika hakijaonyeshwa.

Labda walitoa huduma ya kuhudumia mwili wake kwa manukato.

Hii isingekuwa wakati wa mwisho kwa Shetani kutafuta kumjaribu Yesu.

- Luka 4:13, "*Basi alipomaliza kila jaribu Ibilisi akamwacha akaenda zake kwa muda.*"
- Mat. 16:21-23, "*Tangu wakati huo Yesu alianza kuwaonya wanafunzi wake ya kwamba imempasa kwenda Yerusalemu, na kupata mateso mengi kwa wazee na wakuu wa makuhani, na wandishi na kuuawa, na siku ya tatu kufufuka. Petro akamchukua akaanza kumkemea, akisema, hasha Bwana hayo hayatakupata.*

Akageuka akamwambia Petro, nenda nyuma yangu shetani; u kikwazo kwangu; maana huyawazi yaliyo ya Mungu, bali ya wanadamu."

Kwa siku arobaini ya kushinda majaribu nyuma yake, hasa jaribu la kuchukua njia ya mkato katika utawala wake kama Masihi, Yesu sasa aliandaliwa kuanza huduma yake ya wazi.

Uchunguzi gani ambao mtu anaweza kuufanya kuzingatia "Kujaribiwa Kwa Yesu"?

Hapa kuna chache...

Uchunguzi kutoka katika kujaribiwa kwa Yesu

Tuna adui huyo huyo.

Yesu alijaribiwa na ibilisi, kama tunavyojaribiwa.

1 Pet. 5:8-9, "*Mwe na kiasi na kukesha; kwa kuwa mshitaki wenu Ibilisi, kama samba angurumaye, huzungukazunguka, akitafuta mtu ammeze. Nanyi mpingeni huyo, mkiwa thabiti katika imani, mkijua ya kuwa mateso yale yale yanatimizwa kwa ndugu zenu walioko duniani.*"

Ibilisi sasa anapeleka umakini wake kwa wanafunzi wa Kristo.

Ufu. 12:17, "*Joka akamkasirikia yule mwanamke, akaenda zake afanye vita juu ya wazao wake waliosalia, wazishikao amri za Mungu, na kuwa na ushuhuda wa Yesu; naye akasimama juu ya mchanga wa bahari.*"

Hatupaswi kumchukulia rahisi, maana vita ni halisi!

Efe. 6:12, "*Kwa maana kushindana kwetu sisi si juu ya damu na nyama; bali ni juu ya falme na mamlaka, juu ya wakuu wa giza hili, juu ya majeshi ya pepo wabaya katika ulimwengu wa roho.*"

Tuna majaribu kama hayo.

- **Tamaa ya mwili – uzinzi, hasa ukiwa kijana.**
- **Tamaa ya mwili – vitu vya kimwili, hasa ukiwa kwenye umri wa kati.**
- **Kiburi cha uzima – kiburi na ukengeufu – hasa ukiwa mtu mzima.**

Hizi ni lazima tuzishinde, kama tunataka kuwa na pendo la Baba.

1 Yoh. 2:15-16, "*Msiipende dunia wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila*

kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia."

Tuna vifaa vile vile vinavyotusaidia kushinda.

Yesu aliingia katika neon la Mungu, hivyo nasi.

Efe. 6:17, "*Tena ipokeeni chapeo ya wokovu, na upanga wa Roho ambao ni neno la Mungu;*"

Yesu alikuwa na imani katika mpango wa Mungu (ushindi kupitia mateso), tunahitaji ngao ya imani kama hiyo.

- Efe. 6:16, "*Zaidi ya yote mkiitwaa ngao ya imani, ambayo kwa hiyo mtaweza kuizima mishale yote yenye moto ya yule mwovu.*"
- Heb. 10:35-39, "*Basi msiutupe ujasiri wenu, kwa maana unathawabu kuu. Maana mnahitaji saburi, ili kwamba mkiisha kufanya mapenzi ya Mungu mpate ile ahadi. Kwa kuwa bado kitambo kidogo sana, yeye ajaye atakuja, wala hatakawia. Lakini mwenye haki wangu ataishi kwa imani; naye akisitasita, roho yangu haina furaha naye. Lakini sisi hatumo miongoni mwao wasitao na kupotea, bali tumo miongoni mwa hao walio na imani ya kutuokoa roho zetu.*"

Bila shaka Yesu alisali, maana alitufundisha namna ya kutumia maombi katika kushinda majaribu.

Mat. 26:41, "*Kesheni, mwombe, msijemkaingia majaribuni; roho i radhi, lakini mwili ni dhaifu.*"

Neon la Mungu, imani, na sala – katika hizi ibilisi hana nafasi!

Tuna baraka zilezile tunaposhinda.

Yesu alihudumiwa na malaika; malaika watatupeleka nyumbani.

Luka 16:22, "*Ikawa yule maskini alikufa, akachukuliwa na malaika mpaka kifuani kwa Ibrahimu. Yule tajiri naye akafa akazikwa.*"

Yesu alipokea baraka za ajabu mara aliposhinda na kupaa mbinguni. Ametuhaidi baraka kama hizo.

- Ufu. 2:10. "*Usiogope mambo yatakayo kupata; tazama huyo Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima.*"
- Ufu. 2:26-27, "*Na yeye ashindaye na kuyatunza matendo yangu hata mwisho, nitampa mamlaka juu ya mataifa, naye atawachunga*

kwa fimbo ya chuma, kama vyombo vya mfinyanzi vipondwavyo, kama mimi name nilivyopokea kwa Baba yangu."

- Ufu. 3:21, "*Yeye ashindaye nitampa kuketi pamoja nami katikaa kiti change cha enzi, kama mimi nilivyoshinda nikaketi pamoja na Baba yangu katika kiti chake cha enzi.*"

Tunaweza kujifunza masomo mhumu.

Kujikimu kwa mambo ya kimwili hakuwezi kutosha; tunahitaji kujikimu kiroho katikaneno la Mungu.

Tunapopaswa kumwamini Bwana, hatupaswi kujaribu kijinga.

Maandiko yanaweza kudhihakiwa, pia yakatumiwa.

2 Pet. 3:16, "*Vile vile kama na katika nyaraka zake zote pia, akitoa humo habari za mambo hayo; katika nyaraka hizo yamo mambo ambayo ni vigumu kuelewa nayo;na mambo hayo watu wasio na elimu, wasio imara, huyapotoa kama vile wayapotoavyo na maandiko mengine, kwa uvunjifu wao wenyewe.*"

Njia ya kusifu siyo haraka na rahisi, lakini ni ndefu na ngumu.

- Mdo. 14:22, "*Wakifanya imara roho za wanafunzi na kuwaonya wakae katika ile Imani, na ya kwamba imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi.*"

- Rum. 2:7, "*Wale ambao kwa saburi katika kutenda mema wanatafuta utukufu na heshima na kutokuharibika, watapewa uzima wa milele;*"

Hitimisho

Lakini labda ni somo kuu ya kujifunza kwayo "Kujaribiwa Kwa Yesu" ni kwamba tunaye Mkombozi ambaye kwa mambo yote alifanywa kama sisi…

Ili kwamba aweze kuwa mwenye kutuhurumia na kuhani wetu mkuu.

Heb. 2:17, "*Hivyo ilimpasa kufananishwa na ndugu zake katika mambo yote, apate kuwa kuhani mkuu mwenye rehema, mwaminifu katika mambo ya Mungu, ili afanye suluhu kwa dhambi za watu wake.*"

Baada ya kuteseka, baada ya kujaribiwa, anaweza kutusaidia sisi tunaojaribiwa.

Heb. 2:18, "*Na kwa kuwa mwenyewe aliteswa alipojaribiwa, aweza kuwasaidia wao wanaojaribiwa.*"

Ili kwamba aweze kuwa mwenye huruma, akitoa neema ili isaidie wakati wa mahitaji.

Heb 4:15-16, "*Kwa kuwa hamna kuhani mkuu asiyeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu; bali yeye alijaribiwa sawasawa na sisi katika mambo yote bila kufanya dhambi. Basi na tukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri, ili tupewe rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.*"

Je umetingwa na majaribu?

Mtazame Yesu kama mfano wako katika kujifunza jinsi kushinda majaribu katika maisha yako!

Mtazame Yesu kama kuhani wako mkuu unaptaka kumkaribia Mungu katika sala na upokee neema kwa nyakati hizo ulizo kumbana na majaribu!

Kama katika mambo yote, mtazame Yesu, kama mwandishi wa Waebrania anavyotuhimiza...

Heb. 12:2-3, "*Tukimtazama Yesu mwenye kuanzisha na mwenye kutimiza imani yetu; ambaye kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake aliustahimili msalaba na kuidharau aibu, naye ameketi mkono wa kuume wa kiti cha enzi cha Mungu. Maana mtafakarini sana yeye aliyeustahimili mapingamizi makuu namna hii ya watendao dhambi juu ya nafsi zao, msije mkachoka, mkizimia mioyoni mwenu.*"